

TARGETER WINGS

KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI

GREDI 2 - 2021



Wings
007

SHUGHULI ZA KISWAHILI

UFAHAMU, SARUFI NA KUANDIKA

Jina _____

Jinsia: Mvulana Msichana

Jina la shule _____

Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi.

	Swali la 1	Swali la 2	Swali la 3
Idadi ya alama	5	15	10
Alama sahihi			

1. UFAHAMU

(Alama 5)

Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali:

Nina rafiki yangu anayeitwa Kitili. Ana umri wa miaka saba. Yuko katika gredi ya pili. Amewafuga kuku wawili. Akitoka shulenii kila siku yeye huwapa chakula na maji.



- a) Rafiki ya mwandishi anaitwa nani? _____
- b) Ana umri wa miaka mingapi? _____
- c) Yuko katika gredi gani? _____
- d) Ana kuku wangapi? _____
- e) Yeye huwapa nini? _____

2. SARUFI

(Alama 15)

Andika majina ya wanyama hawa.

(Alama 5)



Kamilisha neno lililo kwenye bano kujaza pengo.

(Alama 5)

Kwa mfano: Wewe ulifua nguo. (fua)

- a) Nyinyi _____ mpira. (cheza)
- b) Nyinyi _____ shamba. (lima)
- c) Nyinyi _____ vitabu. (soma)
- d) Wewe _____ nyumba. (panga)
- e) Wewe _____ mto. (vuka)

Tumia huyo au hao kujaza pengo.

(Alama 5)

- a) Mama _____ alituambia tusicheze mbali.
- b) Wahubiri _____ walituombea.
- c) Mwalimu _____ alituambia tuwatii wazazi.
- d) Mwimbaji _____ alitutumbuiza.
- e) Viranja _____ walikutana.

3. KUANDIKA.

(Alama 10)

Andika sentensi hizi kwa herufi ndogo.

- a) BABA ANALIMA. _____
- b) MAMA ANAPIKA. _____
- c) MTOTO AMELALA. _____
- d) MSICHANA ANAFAGIA. _____
- e) MVULANA ANACHEZA. _____